**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 18 Mei, 2021.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

51. MHESHIMIWA JUMA MAKUNGU JUMA (Jimbo la Kijini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna inavyoshughulikia masuala ya dini na kuweka utulivu kwa waumini wake.

(a) Hivi karibuni nimesikia kuwa Zanzibar inamiliki nyumba katika mji mtukufu wa Makka, Je, suala hilo ni ukweli.

(b) Ikiwa ni kweli, Mahujaji wanaotoka Zanzibar, Je, wananufaika vipi na nyumba hiyo.

(c) Kama si kweli, Serikali haioni haja ya kuwa na nyumba ya namna hiyo huko Makka.

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

127. MHESHIMIWA HUDHAIMA MBARAK TAHIR (Nafasi za Vijana) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuweka mazingira mazuri na wezeshi kwa vijana hasa kupitia mikopo na mitaji inayotolewa katika kila Halmashauri, Baraza la Manispaa na Baraza la Mji ili waweze kujikwamua na umasikini,lakini hadi sasa tatizo la ukosefu wa ajira limezidi kuwa kubwa.

(a) Je, fedha zinazopelekwa kwenye mabaraza hayo kwa ajili ya vijana ambazo ni asilimia mbili (2%) zinatolewa kwa vigezo gani.

(b) Je, mpaka sasa Serikali inaweza kutuambia ni vikundi vingapi vimenufaika na asilimia mbili (2%) ya fedha zilizotolewa kutoka 2015 hadi sasa.

(c) Je, Serikali inaweza kutuambia ni vikundi vingapi vya vijana vimeweza kufanya marejesho ya mikopo waliyokopeshwa ili fedha hizo ziweze kuwanufaisha vijana wengine.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

43. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Tunampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa agizo lake la kutaka kufanyiwa mapitio Sheria ambazo zimekwamisha maendeleo na zile ambazo ni kero kwa wananchi. Kwa kuwa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii “ZSSF” imekuwa ikilalamikiwa sana na wafanyakazi.

Je, Serikali ina mpango wowote wa kuifanyia marekebisho Sheria hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

57. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Pamoja na juhudi zinazochukuliwa na Serikali za kujenga madarasa katika skuli mbali mbali hapa Zanzibar, bado kuna tatizo la idadi kubwa ya wanafunzi madarasani katika skuli za msingi na majengo mengi ya skuli za Serikali ni machakavu na kuwa na upungufu wa vifaa.

(a) Je, Serikali imejipanga vipi katika kupunguza idadi ya wanafunzi katika skuli za msingi.

(b) Je, Serikali imepanga kujenga skuli yoyote ndani ya mwaka huu wa fedha.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

11. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani)

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Muhogo ni miongoni mwa mazao maarufu ya chakula katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu. Kwa kuwa kwa kipindi kirefu zao hili lilikuwa likiathiriwa na mdudu anae shambulia majani na hatimae kupoteza rangi asili ya kijani (Chlorophyll) katika zao hilo na hatimae uzalishaji kuwa mdogo na muhogo huo kupoteza kiwango na ladha.

(a) Je, Serikali inalitambua tatizo hili.

(b) Ni lini italipatia ufumbuzi wa kudumu tatizo hili.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

7. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Licha ya kuwepo kwa Tenki la maji safi na salama katika eneo la Mnara wa Mbao. Wananchi wa Jimbo la Mpendae hasa Shehia ya Kilimani na Migombani

wamekuwa katika kadhia ya muda mrefu sana ya kukosa maji.

(a) Je, Serikali kupitia Wizara ya Maji, Nishati na Madini ina mpango gani wa kuwasaidia wananchi hao kuondokana na hali hiyo.

(b) Ni lini Serikali itaunganisha miundombinu ya mabomba ili kuruhusu maji hayo sasa kuteremka katika shehia hizo na wananchi waweze kufaidika

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

101. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Sekta ya mwani ni miongoni mwa Sekta za uchumi zilizoajiri wanawake wengi katika ukanda wa bahari katika nchi yetu kama vile Fumba, Bweleo na Nyamanzi. Kwa kuwa hivi sasa Serikali yetu imekuja na Sera ya Uchumi wa Buluu unaotegemea bahari, umekuwa wakati muafaka kwa wakulima wa mwani hasa akina mama ambao wanapata tabu katika ukulima wao wa mazingira magumu na kupata kazi kubwa na ngumu, huku kipato wanachokipata ni kidogo.

(a) Je, Serikali itatumia mfumo gani kuweza kuwafikia wakulima hao na kuwapa mafunzo ili tija ya kilimo cha mwani ipatikane kuendana na uchumi wa buluu.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza bei ya zao la mwani ili kuinua kipato cha wakulima wa mwani hasa akina mama ili waweze kukidhi mahitaji yao.

(c) Je, kuna takwimu zozote zimewekwa za kuwatambua wakulima wa mwani au vikundi vya ukulima wa mwani hasa akina mama ili viweze kupatiwa fursa mbali mbali zinazohusiana na uchumi wa buluu.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

150. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MANDOBA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kwa kuwa Wizara ya Afya huwa na utaratibu wa kupiga dawa majumbani kwa ajili ya kuondoa malaria katika nchi yetu, hivi karibuni tulishuhudia kufanyika zoezi hilo kwa badhi ya maeneo hapa nchini.

Je, ni kwanini ule mfumo wa zamani wa kupiga dawa nyumba zote hapa nchini haufanyiki tena na badala yake dawa zinapigwa baadhi ya maeneo.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais**,** Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**18 Mei, 2021.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**